**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAJI**

# TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA MAJI YA BONDE LA ZIWA TANGANYIKA

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji anatangaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Tanganyika. Bodi hii inaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Sura ya 331 chini ya Kifungu Na. 22 na Kanuni zake (Uteuzi wa Bodi, 2010). Muda wa Bodi ni miaka mitatu.

## MAJUKUMU YA BODI YA MAJI YA BONDE LA ZIWA TANGANYIKA

(a) Kuandaa mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji, miradi, bajeti na mkakati wa utekelezaji wa Bonde;
(b) Kuunganisha mipango ya Wilaya kwenye mipango ya usimamizi wa rasilimali za maji ya Bonde;
(c) Kutoa miongozo na viwango vya ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(d) Kufuatilia, kutathmini na kuidhinisha ujenzi na matengenezo wa miundombinu ya vyanzo vya maji;
(e) Kukusanya, kuchakata na kuchambua takwimu zinazohusu usimamizi wa rasilimali za maji;
(f) Kutunza na kuboresha tathmini za upatikanaji mahitaji ya rasilimali za maji;
(g) Kuidhinisha, kutoa na kufuta vibali vya kutumia maji na kutiririsha majitaka;
(h) Kutunza Daftari la Maji kulingana na Kifungu cha 78;
(i) Kufuatilia na kutekeleza vibali vya kutumia na kutiririsha majitaka na hatua za kuzuia uchafuzi;
(j) Kutatua migogoro inayohusiana na matumizi ya maji ndani ya Bonde;
(k) Kutekeleza miradi na programu za usimamizi wa rasilimali za maji;
(l) Kuratibu shughuli za kisekta za usimamizi wa rasilimali za maji katika ngazi ya bonde na kuwa kiungo cha mawasiliano kati ya Sekta na watumiaji wa maji kwa ujumla;
(m) Kumshauri Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji kwenye mambo ya kiufundi yanayohusu masuala ya maji shirikishi katika bonde;
(n) Kuteuwa Mwenyekiti na wajumbe wa kamati za dakio na kidakio maji; na
(o) Kutayarisha taarifa juu ya hali ya rasilimali za maji katika Bonde.

**SIFA ZA MWOMBAJI**

Mwombaji wa nafasi hii anatakiwa kuwa na ujuzi na uzoefu katika masuala ya Sekta ya Maji au Sekta zinazohusiana na sekta hiyo. Aidha, awe na ujuzi mahsusi kwenye masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji na asiwe/ asitoke kwenye taasisi ambayo ni mtumiaji mkubwa wa maji (Major Water User).

Maombi yatumwe kwa:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maji,
Mji wa Serikali,
Mtaa wa Maji,
S.L.P. 456,
**40473, DODOMA.**

Nakala ya maombi itumwe kupitia barua pepe**: ps@maji.go.tz**

Maombi yaambatishwe na wasifu wa mwombaji (CV) yenye wadhamini watatu na namba zao za simu. Andika "**Mwenyekiti Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Tanganyika"** nyuma ya bahasha.

Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Ijumaa **tarehe 24 Oktoba** na (sio 13 Oktoba), 2025 saa 09.30 alasiri

Imetolewa na:

**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Maji**